

# **BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**



## **WASIFU WA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

*Imeandaliwa na:*

**Katibu Mtendaji**

**Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**12 Barabara ya Kivukoni**

**S.L.P. 1734 Dar-Es-Salaam**

**Simu: +255 22 2137362**

**Simu/Nukushi: +255 22 2125596**

**Barua Pepe : [nec@uwezeseshaji.go.tz](mailto:nec@uwezeseshaji.go.tz)**

**Tovuti : [www.uwezeshaji.go.tz](http://www.uwezeshaji.go.tz)**

**SEPTEMBER, 2020**

## **Yaliyomo**

<b>1.0. UTANGULIZI .....</b>	<b>3</b>
<b>2.0. URATIBU WA MIFUKO YA UWEZESHAJI .....</b>	<b>3</b>
<b>3.0. MUHTASARI WA MIFUKO INAYORATIBIWA NA BARAZA .....</b>	<b>4</b>
3.1. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA .....	4
3.2. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA .....	5
3.3. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU .....	6
3.4. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .....	7
<b>4.0. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA KWA WALENGWA.....</b>	<b>8</b>
<b>5.0. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA.....</b>	<b>12</b>
5.1. MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI .....	12
5.2. MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI .....	14
<b>6.0. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU.....</b>	<b>15</b>
6.1. MIFUKO ILICHINI YA UMILIKI WA SERIKALI.....	15
6.2. MIFUKO YA RUZUKU INAMILIKIWA NA TAASISI BINAFSI.....	20
<b>7.0. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.....</b>	<b>21</b>
7.1. PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI .....	21
7.2. PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI .....	24

## **1.0. UTANGULIZI**

Mifuko ya uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilianzishwa kwa lengo la kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha pamoja na huduma nyingine za uwezeshaji ili kuwafanya wananchi washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao. Madhumuni mahsusi ya mifuko hii ni pamoja na kutatua changamoto zinazozuia wananchi kutoa mchango katika kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vikwazo vinavyosababisha benki kusita kutoa mikopo kama vile gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo, ukosefu wa utambulisho rasmi, kutokuwa na taarifa muhimu za waombaji mikopo, ukosefu wa dhamana, udhaifu unaowafanya wananchi wasikopesheke, ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, ukosefu wa mitaji ya kuchangia uanzishaji wa miradi nk.

Walengwa wakuu wa mifuko ni wananchi wote nchini Tanzania wanaofanya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya kilimo, mifugo, maliasili na utalii, afya, viwanda na biashara, Ujenzi, Maendeleo ya ardhi, mawasiliano na uchukuzi, nishati, maji na elimu.

## **2.0. URATIBU WA MIFUKO YA UWEZESHAJI**

Uratibu wa mifuko unaofanywa na Baraza unatokana na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa nguzo ya tatu (Upatikanaji wa Mitaji) ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, 2004, Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha ya mwaka 2017 (NMP, 2017) pamoja na Sheria yake ya Mwaka 2018 (MPA, 2018). Aidha, ili kuhakikisha kuwa Baraza linaratibu mifuko ipasavyo, imefanikiwa kuigawa katika makundi makuu manne ambayo ni Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa, Mifuko inayotoa dhamana kwa kushirikiana na Taasisi za fedha, Mifuko inayotoa ruzuku na Programu za Uwezeshaji.

Baraza linaratibu Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa njia zifuatazo:-

- i. Kutunza Daftari la Orodha ya Mifuko ya Uwezeshaji ;
- ii. Kujenga uelewa kwa Umma juu ya uwepo wa Mifuko/Programu za Uwezeshaji na jinsi ya kunufaika na Mifuko hiyo;
- iii. Kuitisha vikao/mikutano na Taasisi za Mifuko/Programu ambapo mikutano hiyo hufanyika mara mbili kwa mwaka au zaidi pale inapobidi;
- iv. Kupokea taarifa za Mifuko, kuzipitia na kuandaa taarifa ya pamoja;
- v. Kuwaunganisha wananchi na Mifuko ya Uwezeshaji; na
- vi. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma na matokeo ya uwezeshaji kupitia mifuko na program za uwezeshaji.

### 3.0. MUHTASARI WA MIFUKO INAYORATIBIWA NA BARAZA

#### 3.1. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA

##### MFUKO INAYOTOA HUDUMA

1. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund –WDF)
2. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund –NEDF)
3. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (Agricultural Inputs Trust Fund –AGITF)
4. Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund)
5. Mfuko wa Kilimo Kwanza (Kilimo Kwanza Fund–KKCF)
6. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu
7. Mfuko wa Mzunguko katika mikoa (SIDO RRF)
8. Mfuko wa Usambazi wa Maji kwa Umeme wa Jua
9. Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu
10. Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali
11. Mfuko wa Uhamisishaji wa matumizi ya ethanol kama nishati mbadala ya kupikia
12. Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji (Irrigation Development Fund-IDF)
13. Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund – GCF)
14. Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Serikali Kuu (Public Service Advances Fund)

##### MIFUKO INAYOFUATILIA MAREJESHO

15. Mfuko wa Ufilisi wa Benki ya Nyumba (THB)
16. Mfuko wa Japan wa Uagizaji bidhaa kutoka nje (Commodity Import Support- CIS)
17. Mfuko wa kusaidia Kilimo cha Maua – (Floriculture Financing).
18. Mfuko wa kusaidia Kiwanda cha Nyama cha SAAFI Ltd.

### 3.2. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA

MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI	MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI
<p style="text-align: center;"><b>MIFUKO INAYOTOA HUDUMA</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme –ECGS)</li> <li>2. Mfuko wa dhamana za mikopo kwa wakulima wadogowadogo (Smallholders’ Credit Guarantee Scheme)</li> <li>3. Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund –CAF)</li> <li>4. Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Miradi Midogo na ya Kati (SME-CGS)</li> <li>5. Mfuko wa Nishati Jadiifu (TANZANIA Energy Development and Expansion- TEDAP)</li> <li>6. Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (Housing Microfinance Fund)</li> <li>7. Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamli katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME –CGS)</li> </ol> <p style="text-align: center;"><b>MIFUKO INAYOFUATILIA MAREJESHO</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>8. Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund –MEF)</li> <li>9. Mfuko wa Kupambana na Umasikini na Kuongeza Ajira (JK Fund)</li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Private Agricultural Sector Support Trust –PASS Trust)</li> <li>2. Asasi ya Kusaidia Wajasiriamali Wadogo na Wakati (African Guarantee Fund)</li> <li>3. Asasi ya Kusaidia na kuboresha huduma ya afya kwa jamii (Medicla Credit Fund)</li> <li>4. African Trade Insurance</li> </ol>

### 3.3. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU

MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI	MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund –REF)</li> <li>2. Bodi ya Mfuko wa Barabara</li> <li>3. SAGCOT-CTF</li> <li>4. Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF)</li> <li>5. Mfuko wa Elimu Tanzania (Tanzania Education Fund –TEF)</li> <li>6. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund –TASAF)</li> <li>7. Mfuko wa Kuongeza Ujuzi na Stadi za Kazi (SDF)</li> <li>8. Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund –TaFF)</li> <li>9. Mfuko wa Fidia ya Ardhi Tanzania (Land Compensation Fund-LCF)</li> <li>10. Mfuko wa Ubunifu Vijijini ( Rural Innovation Fund-RIF)</li> <li>11. Mfuko wa Taifa wa Maji (National Water Fund - NWF)</li> <li>12. Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF)</li> <li>13. Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund-EAMCEF)</li> <li>14. Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund For Antiquities)</li> <li>15. Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL)</li> <li>16. Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa</li> <li>17. Mfuko wa Udhadini wa Kudhibiti Ukimwi (Aids Trust Fund-ATF)</li> <li>18. Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika</li> <li>19. Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira</li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Women Trust Fund-Trust (WFT-Trust)</li> <li>2. Social Action Trust Fund(SATF)</li> </ol>

### 3.4. PROGRAMU ZA UWEZESHaji WANANCHI KIUCHUMI

PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI	PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Mafunzo ya Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara</li> <li>2. Mafunzo ya Stadi za Ujuzi</li> <li>3. Mpango wa Kuhamasisha na kukuza Moyo wa Kujitolea miongoni mwa Vijana</li> <li>4. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)</li> <li>5. Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme)</li> <li>6. Mpango wa Mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi (Internship training)</li> <li>7. Mpango wa kutambua na kurasimisha ujuzi wa vijana uliopatikana nje ya mfumo rasmi (<i>Recognition of Prior Learning</i>)</li> <li>8. Mpango wa kuwawezesha vijana kushiriki katika kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba</li> <li>9. Mpango wa kuwapatia vijana mafunzo ya kilimo nchini Israel</li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Mfuko wa Kuendeleza Sekta Binafsi za Fedha Tanzania (Financial Sector Deepening Trust- FSdT)</li> <li>2. Kituo cha Ubunifu wa Kilimo Biashara (AIC)</li> <li>3. Mpango wa Kuendeleza Vijana na Wanawake</li> </ol>

#### 4.0. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA KWA WALENGWA

*Mifuko katika Kundi hili yote iko chini ya umiliki wa Serikali*

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (Youth Development Fund – YDF);	Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi,Vijana,Ajira na wenye Ulemavu),	kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali	Vijana wote wa Kike na Kiume walio katika vikundi vya uzalishaji mali wenye umri kati ya Miaka 15 hadi 35
2	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund – WDF)	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	kutoa mikopo yenye masharti nafuu hasa kwa wanawake wasio na vigezo au sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha ili waweze kujikwamua kiuchumi na kupambana na Changamoto mbalimbali zinazowakabili kulingana na nafasi yao katika family na jamii	Wanawake wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na wasichana wenye umri chini ya miaka 18 wenye watoto.
3	Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund – NEDF)	Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo(SIDO)	Kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara, kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi	Wajasiriamali Wadogo na wakati wenye Viwanda vidogo na Wafanyabiashara Wadogo
4	Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (Agricultural Inputs Trust Fund – AGITF)	Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (Agricultural Inputs Trust Fund –AGITF)	Upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Wakulima, Wafugaji na Wavuvi mmoja mmoja na vikundi (AMCOS, SACCOS.);</li> <li>ii. Mawakala binafsi wanaosambaza pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi;</li> <li>iii. Mashirika na Taasisi za Jamii, zinazojishughulisha na kilimo; na</li> <li>iv. Benki za wananchi na Ushirika ambazo</li> </ul>

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
				hutoa mikopo moja kwa moja kwa wakulima katika maeneo ambayo zipo kwa niaba ya Mfuko wa Pembejeo.
5	Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund)	SELF Microfinance Fund	Kutoa mikopo ya jumla ( <i>wholesale lending</i> ) ya masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo kupitia Asasi ndogo na za Kati za kifedha	Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo – (SACCOS), Benki za Wananchi (Community Banks); Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Kampuni za fedha zinazotoa huduma za mikopo (Microfinance Companies).
6	Mfuko wa Kilimo Kwanza (Kilimo Kwanza Fund–KKCF)	Benki ya Maendeleo ya TIB	Kukuza sekta ya kilimo na kuwawezesha wakulima kupata fedha kwa unafuu ili kuendeleza Kilimo.	Wakulima Wadogo na wa Kati Taasisi Ndogo za fedha na vyama vya ushirika (SACCOS)
7	Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)	Kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye uhitaji na sifa stahili.	Wanafunzi wanaotegemea kujiunga na Vyuo vya elimu ya Juu
8	Mfuko wa Mzunguko katika mikoa (SIDO RRF)	Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)	Kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara, kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi	Wajasiriamali Wadogo na Wakati wenye Viwanda vidogo na Wafanyabiashara Wadogo
9	Mfuko wa Usambazi wa Maji kwa Umeme wa Jua	Benki ya Maendeleo ya TIB	kusaidia jumuiya za watumia maji kutoka kwenye mfumo wa kutumia diseli kama chanzo cha nishati na kwenda kutumia umeme jua kwa ajili ya kusukuma maji ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji maji safi na salama	Jumuiya ya Watua maji kutoka Mikoa ya Dodoma, Singida, Mtwara, Shinyanga, Tabora, Kagera, Mara, na Lind

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
10	Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu	Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu)	Kuondoa uhusiano uliopo baina ya ulemavu na unaskini kwa kuwezesha wenye ulemavu kujikwamua kiuchumi	Watu wote wenye ulemavu wanaoishi Tanzania Bara bila kujali umri,jinsia, rangi aina ya ulemavu, vyama vya watu wenye Ulemavu, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA)
11	Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	Kujenga, Kukarabati au Kununua Nyumba	Watumishi wakudumu wa Serikali
12	Mfuko wa Uhamisishaji wa matumizi ya ethanol kama nishati mbadala ya kupikia	TIB Development	Kutoa mikopo ya Kuhamasisha matumizi mbadala ya Nishati kwa ajili ya kupikia	Wananchi Wote
13	Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji (Irrigation Development Fund-IDF)	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	Kuchochea maendeleo endelevu ya sekta ya umwagiliaji kwa kutoa mikopo na ruzuku	Wananchi wanajishughulisha na kilimo cha Umwagiliaji
14	Mfuko wa Ufilisi wa Benki ya Nyumba (THB)	TIB Development	Kuwapatia hati miliki wateja wote waliomaliza mikopo yao na ambao hawakubahatika kupata mikopo na walikuwa wamewasilisha hatimiliki zao na Kukusanya marejesho ya mikopo toka kwa wakopaji	Walengwa wa ufilisi ni wale walio na mikopo na hati kwa iliyokuwa THB

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
15	Mfuko wa Japan wa Uagizaji bidhaa kutoka nje (Commodity Import Support-CSI)	TIB Development	Kusaidia uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi katika sekta kipaumbele (Kilimo, Viwanda Vidogo, Ujenzi, Nishati, Uvuvi, Madini, Usafilishaji, Afya na Elimu)	Wananchi walio katika sekta kipaumbele kilimo, viwanda vidogo, ujenzi, nishati uvuvi, madini, usafirishaji, afya na elimu
16	Mfuko wa kusaidia Kilimo cha Maua – (Floriculture Financing).	TIB Development	Kuuzua maua ndani na nje ya nchi ili kuwezesha wakulima kuongeza uzalishaji na uuzaji wa mbogamboga na maua ndani na nje ya nchi ili kuliongezea taifa fedha za kigeni na kuinua uchumi kwa ujumla.	Wananchi walio katika sekta ya kilimo cha Maua na mbogamboga.
17	Mfuko wa kusaidia Kiwanda cha Nyama cha SAAFI Ltd.	TIB Development	Kusimamia uendeshaji wa kiwanda cha Nyama kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi	Kiwanda cha nyama cha SAAFI Ltd kilichopo Mkoani Rukwa.
18	Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund – GCF)	Ofisi ya Makamu wa Rais (VPO)	Umelenga upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa miradi inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi	Miradi yenye kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi
19	Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Serikali Kuu (Public Service Advances Fund)	Wizara ya Fedha na Mipango	Madhumuni ya Mfuko huu ni kuboresha maisha ya watumishi wa Serikali Kuu kwa njia ya mikopo ya ununuzi wa vyombo vya usafiri na vifaa vya nyumbani	Watumishi wa Serikali walio katika ajira ya kudumu

## 5.0. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA

### 5.1. MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme – ECGS)	Benki Kuu ya Tanzania	Kudhamini wauzaji wa bidhaa nje ya nchi wenye uhitaji ili kuhamasisha benki na taasisi za fedha kutoa mikopo kwa sekta ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi, hususani wauzaji wa bidhaa zisizo za jadi, ili kupanua wigo wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi kwa lengo la kukuza mapato.	Wakopaji wote wenye miradi ya maendeleo yenye lengo la kuzalisha na kuuza bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi
2	Mfuko wa Uwezesaji wa Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund – MEF)	Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi	Kuondoa vikwazo vinavyosababisha ukosefu wa mitaji na mikopo kwa wananchi wajasiriamali.	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Watu binafsi</li> <li>ii. Wajasiriamali katika VICOBA</li> <li>iii. Wajasiriamali katika SACCOS</li> <li>iv. Wajasiriamali katika vikundi vingine vya kiuchumi na taasisi mbalimbali</li> </ul>
3	Mfuko wa dhamana za mikopo kwa wakulima wadogowadogo (Smallholders' Credit Guarantee Scheme)	Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)	Kuhamasisha mabanki ya kibiashara kuongeza mikopo yao kwa wakulima wadogo wadogo ambao wamesahaulika kwenye huduma rasmi za kibenki	Wakulima Wadogo Wadogo
4	Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF)	Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB)	Kusaidia Makandarasi wazalendo wadogo na wa kati kuweza kupata dhamana za zabuni na malipo ya wawali kama njia ya kuwawezesha kushiriki katika kazi za ujenzi.	Walengwa wakuu wa mfuko huu ni Makandarasi wazalendo wa madaraja ya VII - IV kwa kazi za kawaida na daraja la III – II kwa kazi maalumu

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
5	Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Miradi Midogo na ya Kati (SME-CGS)	Benki Kuu ya Tanzania	Kuendeleza miradi midogo na ya kati (SMEs) kwa kujenga mazingira ya kuwezesha wajasiriamali wenye miradi midogo na ya kati kupata mitaji kwa njia ya mikopo ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika ukuaji wa uchumi.	Wajasiriamali wenye miradi midogo na ya kati
6	Mfuko wa Nishati Jadiifu (TANZANIA Energy Development and Expansion-TEDAP)	Benki ya Maendeleo ya TIB	Kuwezesha upatikanaji wa umeme uliozalishwa kutokana na maji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania	Taasisi za Kifedha, Wakulima Wadogo wadogo na wa kati, Wafanyabiashara na Wananchi wa kawaida.
7	Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (Housing Microfinance Fund)	Benki Kuu ya Tanzania (BOT),	Kujenga mfumo endelevu wa mikopo ya nyumba za makazi kupitia sekta ya benki ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba za makazi kwa wananchi wa kipato cha kati na cha chini	Watanzania wote
8	Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamali katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME –CGS)	Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)	kuendeleza miradi yao ya Sekta ya uzalishaji wa mazao ya Kilimo (Agro Processing)	Walengwa wa mikopo ni wajasiriamali wadogo na wa kati walioko kwenye sekta ya uzalishaji wa mazao ya kilimo waliowahi kunufaika na huduma zinazotolewa na SIDO
9	Mfuko wa Kupambana na Umasikini na Kuongeza Ajira (JK Fund);	Benki Kuu ya Tanzania	Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa kutumia taratibu za kibenki kuwawezesha wananchi kiuchumi, wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati (micro, small and middle entrepreneurs), wajasiriamali wa vijijini na mijini ili kuanzisha na kuendeleza miradi inayolenga kuongeza kipato, tija na fursa za ajira	Wajasiriamali wadogo na wa kati

## 5.2. MIFUKO ILIYOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Private Agricultural Sector Support Trust –PASS Trust)	Mfuko wa Sekta Binafsi za Kilimo	Kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara na sekta zinazohusika	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Watu binafsi wanao fanyabiashara za kilimo, ufugaji na uvuvi</li> <li>ii. Vikundi na vyama vya wakulima wafugaji na wavuvi vilivyosajiliwa; na</li> <li>iii. Kampuni zinazo jishughulisha na miradi mbalimbali katika mnyororo wathamani wakilimo (Mazao, Mifugo na Uvuvi)</li> </ul>
2	Asasi ya Kusaidia Wajasiriamali Wadogo na Wakati (African Guarantee Fund)	NMB - African Guarantee Fund	Kusaidia wafanyabiashara wa kati na wadogo kukuza biashara zao na kuongeza thamani ya bidhaa katika Bara la Afrika	Watu binafsi na makampuni yanajisughulisha na usafirishaji, uzalishaji, na sekta mbalimbali za biashara , utalii, afya na elimu
3	Asasi ya Kusaidia na kuboresha huduma ya afya kwa jamii(Medicla Credit Fund)	NMB - Medicla Credit Fund	Kusaidia sekta ya afya ili kuwezesha upatikanaji wa vifaa tiba na majengo	Watu binafsi na makampuni yanayojishughulisha na sekta ya afya kama ujenzi wa hospitali, maduka ya dawa, maabara n.k
4	African Trade Insurance	NMB - African Trade Insurance	Kusaidia wafanyabiashara wadogo, Wakubwa na Wakati katika kukuza biashara zao, kuongeza ajira na thamani ya bidhaa katika Baraz la Afrika	Kampuni binafsi na za Serikali zinazojishughulisha na nishati,ujenzi, miundombinu, kilimo na uzalishaji

## 6.0. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU

### 6.1. MIFUKO ILICHINI YA UMILIKI WA SERIKALI

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund –REF)	Wakala ya Nishati Vijijini (REA)	Kuwezesha, Kuratibu, na Kuhamasisha uwekezaji na uendelezaji wa miradi ya nishati bora vijijini	Makazi ya wananchi waishio Vijijini, Maeneo ya Biashara vijijini, Taasisi za Umma kama vile vituo vya Polisi, Shule za Msingi na Sekondari zilizopo vijijini, Pampu na Visima vya Maji vijijini, Shughuli za Uzalishaji Mali, Masamba ya Umwagiliaji
2	Bodi ya Mfuko wa Barabara	Bodi ya Mfuko wa Barabara(RFB)	kuhakikisha kunakuwa na fedha na usimamizi wa kutosha za matengenezo ya barabara Mijini na Vijijini	TANROADS na TARURA
3	SAGCOT-CTF	SAGCOT-CTF	Kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kama soko kuu la mazao ya wakulima wadogo na kuwekeza katika kutatua changamoto za kilimo biashara	Wakulima wakubwa , Wakati na Wadogo
4	Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF)	Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF)	Kuleta msukumo na ushiriki wa watoa huduma za mawasiliano katika kukuza na kusukuma maendeleo ya kijamii na uchumi kwa kutumia mawasiliano hususani katika maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayana mvuto wa	Wakazi wa Maeneo ya Vijijini na Shule

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
			kibiashara.	
<b>5</b>	Mfuko wa Elimu Tanzania (Tanzania Education Fund – TEF)	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)	Kuongeza nguvu za serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa Elimu na upatikanaji wake kwa usawa.	Taasisi zote za elimu zilizosajiliwa katika ngazi zote za elimu kwa upande wa Tanzania Bara na zile za elimu ya juu kwa upande wa Tanzania Visiwani
<b>6</b>	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF)	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF)	kusaidia jamii na wananchi ambao wameathirika zaidi na umaskini na wanaoishi katika mazingira hatarishi ili waweze kujikwamua na hatimaye kutoka katika hali hiyo	Kaya maskini
<b>8</b>	Mfuko wa Kuongeza Ujuzi na Stadi za Kazi (SDF)	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)	Kukuza na kuendeleza ujuzi katika sekta za kilimo-uchumi, utalii na huduma za ukarimu, uchukuzi, ujenzi, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), na Nishati.	Wanawake, Vijana na makundi maalum kama yatima na wenye ulemavu
<b>9</b>	Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund –TaFF)	Mfuko wa Misitu Tanzania	Kutoa ruzuku kwa wadau wanaojihusisha na uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali misitu kupitia uwezeshwaji wa fedha, vifaa na/au utalaam.	Watu binafsi; Vikundi vya Jamii; asasi zisizo za kiserikali; Jumuiya/Taasisi za Kidini; Asasi/Taasisi za Mafunzo; Taasisi za Utafiti; Wizara, Idara, na Wakala za Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu katika Mikoa ya Tanzania Bara.

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
<b>9</b>	Mfuko wa Fidia ya Ardhi Tanzania	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,	Kuratibu masuala yote ya ulipaji wa fidia ya ardhi	Mmiliki wa ardhi ambaye anaondolewa kwenye eneo lake lililotwaliwa kwa manufaa ya umma na kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa.
<b>10</b>	Mfuko wa Ubunifu Vijijini (RIF)	Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)	Kuongeza wigo wa maendeleo kwa kufadhili juhudi na mipango inayochagiza ubunifu katika kutatua changamoto mbalimbali zinazomkabili mkulima vijijini	Watu binafsi; Watoa huduma za kifedha, ikiwa ni pamoja na taasisi za fedha za maendeleo (DFIs), benki, MFIs, SACCOS, nk; Mitandao ya FSPs; makampuni yanayotoa huduma za teknolojia; Makampuni ya biashara ya kilimo; Vikundi vya wakulima / Mashirika ya wazalishaji; Taasisi za kitaaluma / utafiti; Mashirika yasiyo ya Serikali / Mashirika ya Kijamii
<b>11</b>	Mfuko wa Taifa wa Maji (National Water Fund - NWF)	Wizara ya Maji	Kutekeleza miradi ya maji vijijini, upanuzi, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji katika maeneo ya mijini hususan kwenye miji midogo ya wilaya na miradi ya Kitaifa, pamoja na miradi ya uhifadhi wa vyanzo vya maji katika mabonde ya maji nchini.	Miradi ya Maji Vijijini
<b>12</b>	Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF)	Wizara ya Maliasili na Utalii	Kuwezesha jitihada za serikali za kupambana na ujangili na biashara haramu za wanyamapori pamoja na kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu uhifadhi na kuchangia huduma za jamii kama vile Elimu, Afya, Maji, nk kwenye vijiji vilivyo	Jamii zinazozunguka hifadhi, vikundi vya Kupambana na ujangili, Shule, Vituo vya Afya na Maji .

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
			karibu na Mapori ya Akiba.	
13	Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund-EAMCEF)	Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund-EAMCEF)	Kuhifadhi bioanuwai ya misitu iliyomo katika Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania, kupunguza umaskini wa jamii zinazoishi kandokando ya milima hii muhimu pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi	Wanajamii, Idara za Serikali, Halmashauri za Wilaya, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za utafiti
14	Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund For Antiquities)	Wizara ya Maliasili na Utalii	Kuwezesha shughuli za utafiti, uhifadhi na uendelezaji wa malikale	Vituo vya Malekale
15	Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL)	Wizara ya Maliasili na Utalii	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Kuendeleza mazao ya Utalii, kudhibiti ubora wa huduma za biashara za Utalii;</li> <li>ii. Kukuza na kutangaza vivutio vya Utalii;</li> <li>iii. Kujenga uwezo katika sekta ya Utalii; na</li> <li>iv. Kufanya tafiti katika Sekta ya Utalii;</li> </ul>	Idara/Taasisi zinazofaidika na tozo hiyo ni pamoja na Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania na Chuo cha Taifa cha Utalii
16	Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa	Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo	Kuwasaidia wasanii kujiendeleza kiuchumi kupitia masuala mbalimbali nje ya sanaa.	Wasanii katika maeneo mbalimbali

<b>Na</b>	<b>JINA LA MFUKO</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
17	Mfuko wa Udhadini wa Kudhibiti Ukimwi (Aids Trust Fund-ATF)	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS)	Kuboresha elimu ya matibabu ya dawa za kufubaza VVU na pamoja na kuhamasisha wananchi kupima VVU na kuwaunganisha kwenye huduma za matibabu.	Wananchi walioathirika na VVU
18	Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika	Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika (TCDC)	Kuratibu shughuli zote za mafunzo kwa wanachama, Bodi za Uongozi wa Vyama pamoja na Watendaji, kugharamia uwezesaji na upatikanaji wa vifaa vya mafunzo na shughuli za utafiti katika sekta ya Ushirika kwa ujumla.	Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo
19	Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)	Kuwezesha kufanyika utafiti unaolenga kuboresha mahitaji ya usimamizi wa mazingira, kutoa tuzo za uhifadhi wa mazingira, kutoa ufadhili wa masomo ya ngazi za juu nakuboresha na kusaidia kupitia ruzuku programu za usimamizi wa mazingira za jumuiya	Miradi yenye kuboresha mazingira

## 6.2. MIFUKO YA RUZUKU INAMILIKIWA NA TAASISI BINAFSI

Na	JINA LA MFUKO	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Women Trust Fund-Trust	Women Trust Fund-Trust	Kuwawezesha wanawake na wasichana kupata elimu, kuwajengea uwezo ili wawe viongozi wazuri pamoja na kutoa ruzuku (wanayo kamati maalum inayopitia maombi ya ruzuku).	Wanawake na Wasichana
2	Social Action Trust Fund		kusaidia watoto walio katika mazingira magumu zaidi (MVC) na kushughulikia athari iliyosababishwa na VVU / Ukimwi na umasikini nchini Tanzania. Hii inafanikiwa kupitia utoaji wa misaada kwa NGOs, FBOs na CBOs zilizosajiliwa nchini Tanzania.	NGOs, FBOs na CBOs

## 7.0. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### 7.1. PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA SERIKALI

Na	JINA PROGRAMU	LA	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mafunzo ya Ujasiriamali Usimamizi Biashara	ya na wa	Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kutoa elimu ya Ujasiriamali na Usimamizi wa biashara kwa vijana ambao wamejiajiri katika sekta isiyo rasmi ili waweze kukuza na kuendeleza shughuli zao kwa weledi zaidi.	Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35
2	Mafunzo ya Stadi za Ujuzi		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kuwapatia vijana walioko nje ya shule stadi za ujuzi mbalimbali zitakazowawezesha kujajiri na kujipatia kipato (Mfano Ufundi Uashe, Ufundi Magari, Ufundi Umeme, Mapishi n.k)	Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35
3	Mpango wa Kuhamasisha kukuza Moyo wa Kujitolea miongoni mwa Vijana	wa na wa	Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kujenga ari ya kujitolea miongoni mwa vijana pamoja na kuwa na makambi kazi (Work Camp) ya vijana ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kujitolea na ushiriki wa shughuli za kijamii	Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35
4	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)	wa za	MKURABITA	Kuwawezesha wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara kushiriki katika uchumi rasmi unaosimamiwa na utawala wa sheria. Hii ni pamoja na kuzitumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana	Wananchi wa mijini na vijijini wanaomiliki rasilimali nje ya mfumo unaotambulika kisheria na wanaoendesha biashara bila kukidhi matakwa ya kisheria.

Na	JINA PROGRAMU	LA	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
				katika kupata mikopo na fursa zinginezo zilizoko katika uchumi wa soko.	
5	Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme)		SIDO, Benki ya Azania, VETA, NEEC na NSSF	kutatua changamoto ya upatikanaji wa mitaji katika miradi ya Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) iliyo katika sekta ya kilimo, Ufugaji na Uvuvi hususan katika eneo la kuongeza mnyororo wa thamani la kuchakata mazao ya kilimo	Miradi midogo na ya Kati
6	Mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi kwa wahitimu Mpango wa Mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi (Internship training)		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kuwaandaa vijana waliohitimu mafunzo ya elimu ya juu kwa kuwapa ujuzi wa elimu kwa vitendo.	Vijana umri wa miaka 15 – 35 na Wahitimu wa vyuo
7	Mpango wa kutambua na kurasimisha ujuzi wa vijana uliopatikana nje ya mfumo rasmi ( <i>Recognition of Prior Learning</i> )		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kutambua vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi ili waweze kufanya kazi katika sekta rasmi kutokana na utambulisho wa ujuzi wao.	Vijana wenye uzoefu usiopungua miaka 5 kwenye fani anayoifanya
8	Mpango wa Ubunifu na Ujasiriamali kwa vijana		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kutambua uwezo na mchango wa vijana katika shughuli za kiuchumi na kijamii	Vijana wenye umri wa miaka 15-35 ambao wenye talanta ya ubunifu

<b>Na</b>	<b>JINA PROGRAMU</b>	<b>LA</b>	<b>TAASISI SIMAMIZI</b>	<b>MADHUMUNI</b>	<b>WALENGWA</b>
9	Mpango wa kuwawezesha vijana kushiriki katika kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kuwajengea vijana ujuzi katika shughuli za kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya Kitalu Nyumba ili kuongeza tija	Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35
10	Mpango wa kuwapatia vijana mafunzo ya kilimo nchini Israel		Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU)	Kuwapatia vijana ujuzi wa kuendesha kilimo cha Kisasa ili kukidhi soko la bidhaa za Kilimo	Vijana wenye umri wa miaka 15 - 35

## 7.2. PROGRAMU ZILIZOCHINI YA UMILIKI WA TAASISI BINAFSI

Na	JINA LA PROGRAMU	TAASISI SIMAMIZI	MADHUMUNI	WALENGWA
1	Mfuko wa Kuendeleza Sekta Binafsi za Fedha Tanzania (Financial Sector Deepening Trust- FSDT)	Mfuko wa Kuendeleza Sekta Binafsi za Fedha Tanzania (Financial Sector Deepening Trust- FSDT)	Kuhakikisha kuna upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha unaongezeka na kuwa endelevu ili Watanzania wengi wapate fursa ya kuzitumia huduma bora za kifedha kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao, kuongeza tija katika uzalishaji na ujasiriamali, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.	Wananchi wote na Watoa Huduma za Kifedha
2	Kituo cha Ubunifu wa Kilimo Biashara (AIC)	PASS Trust	Kusaidia ukuaji wa kilimo biashara kwa kuongeza ufanisi na tija ili kukuza ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa kwa	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Kampuni, ushirika au mtu binafsi ambaye amepita awamu ya uanzishaji wa kilimo biashara na anaweza kuonesha uwezekano wa biashara kukua.</li> <li>ii. Wahitimu wa vyuo na vijana wengine wenye mawazo bunifu ya kilimo biashara wanaochaguliwa kujiunga na kituo cha kutamia vijana (Incubation Center).</li> <li>iii. Makampuni au wamiliki wa kilimo biashara yenye matatizo na zinazoyumba au kueleka kufungwa sokoni kutokana na sababu mbalimbali.</li> <li>iv. Wanawake wajasiriamali kwenye kilimo biashara.</li> </ul>
3	Mpango wa Kuendeleza Vijana na Wanawake	KCB Bank	Kutoa mafunzo ya ujuzi kwa Vijana na Wanawake	Wanawake na Vijana